**TRA SACCOS LIMITED**

**SERA YA HISA NA AKIBA**

**Marejeo ya Januari, 2022**

**YALIYOMO**

SEHEMU YA KWANZA: DIRA, DHAMIRA NA MWELEKEO ........ 4
1.1. Utangulizi ........ 4
1.2. Sera ya Hisa na Akiba........ 4
1.3. Dira, Dhamira na Maadili ya Msingi ........ 4
1.3.1. Dira ........ 4
1.3.2. Dhamira ........ 4
1.3.3. Maadili Ya Msingi ........ 4
SEHEMU YA PILI: MADHUMUNI NA MSINGI WA SERA YA HISA NA AKIBA........ 6
2.1. Madhumuni ya Sera ........ 6
2.2. Msingi wa Sera ........ 6
2.3. Wigo wa Sera........ 7
2.4. Marekebisho ya Sera........ 7
SEHEMU YA TATU: HISA ........ 8
3.1 Umiliki wa Hisa........ 8
3.2 Kiwango cha Chini cha Hisa za Uanachama ........ 8
3.3 Utaratibu wa Ununuzi wa Hisa ........ 8
3.4 Uendeshaji wa Akaunti ya Hisa........ 8
3.5 Kuhamisha Hisa........ 9
3.6 Katazo la Kutumia Hisa kama Dhamana........ 9
3.7 Kurejeshewa Hisa ........ 9
3.8 Tathimini ya Thamani ya Hisa........ 9
SEHEMU YA NNE: AKIBA ........ 10
4.1 Aina ya Akiba Katika Chama........ 10
4.2 Akiba ya Lazima........ 10

4.2.1 Uhamasishaji ........................................................................................ 10
4.2.2 Utaratibu wa Uchangiaji ............................................................................ 10
4.2.3 Riba Juu ya Akiba ...................................................................................... 11
4.2.5 Uendeshaji wa Akaunti ya Akiba ya Lazima .............................................. 11
4.2.6 Dhamana ..................................................................................................... 12
4.2.7 Kurejeshewa Akiba ..................................................................................... 12
4.3 Akiba za Hiari ................................................................................................. 12
4.3.1 Akiba ya Kustaafu ....................................................................................... 13
4.3.2 Akiba ya Elimu ............................................................................................ 15
4.3.3 Akiba ya Afya .............................................................................................. 17
4.3.4 Akiba ya Wekeza ......................................................................................... 19
5.0 Wanachama Wanaojitoa Katika Chama ......................................................... 21
5.1 Faida Anazopoteza Mwanachama Aliyejitoa .................................................. 22
6.0 Wanachama Waliosinzia ................................................................................ 22
Jedwali namba 1 ................................................................................................. 23

**SEHEMU YA KWANZA**

**DIRA, DHAMIRA NA MWELEKEO**

## 1.1. Utangulizi

TRA SACCOS LTD ni Chama cha Akiba na Mikopo kilichoanzishwa na wafanyakazi wa Mamlaka kwa lengo la kuwahudumia Wanachama wake kwa kuwapatia huduma mbalimbali za kifedha ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi, kijamii na ya kimazingira kwa kufuata taratibu za kidemokrasia, misingi, Kanuni na Sheria ya Vyama vya Ushirika pamoja na Masharti ya Chama. Bodi ya Chama imeendelea kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za vyama vya Ushirika, Masharti ya Chama na Sera mbalimbali kama zinavyoidhinishwa na Wanachama ili kuhakikisha kwamba Chama kinaendeshwa kwa ufanisi na kwa kuzingatia taratibu na uwezo wa Chama.

## 1.2. Sera ya Hisa na Akiba

Bodi ya Chama katika kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwemo uandaaji na utekelezaji wa Sera mbalimbali kwa lengo la kukiendesha Chama kwa ufanisi na misingi ya Utawala Bora, imeandaa Sera ya Hisa na Akiba

## 1.3. Dira, Dhamira na Maadili ya Msingi

### 1.3.1. Dira

Kuwa Chama cha Akiba na Mikopo cha Kuigwa na cha kisasa nchini Tanzania

### 1.3.2. Dhamira

Kuinua, kustawisha na kuboresha hali ya Kiuchumi na kijamii kwa Wanachama, kwa kuwahamasisha kuweka akiba na kuwapatia Mikopo yenye Manufaa na riba nafuu pamoja na huduma zingine za kifedha kwa kutumia mfumo wa teknolojia ya kisasa.

### 1.3.3. Maadili Ya Msingi

a) Kutoa huduma nzuri na zenye ufanisi kwa Wanachama kwa Uadilifu, Uaminifu, Haki na Usawa.

b) Kubuni, kuboresha na kuendeleza huduma bora kwa Wanachama

c) Kutumia utaalamu katika Uongozi na Kufuata misingi ya Utawala bora.

d) Kuendesha Chama kwa weledi na uwajibikaji.

## SEHEMU YA PILI

## MADHUMUNI NA MSINGI WA SERA YA HISA NA AKIBA

### 2.1. Madhumuni ya Sera

Madhumuni ya sera hii ni kuweka mfumo madhubuti wa utoaji huduma na usimamizi wa Hisa na Akiba kwa Wanachama ili kuweka uwazi na uwajibikaji kwa viongozi na Wanachama.

Sera hii imeandaliwa kwa ajili ya kuweka utaratibu ulio bora wa kupokea Hisa na Akiba kutoka kwa Wanachama, kuzisimamia na kuzirejesha kwa Wanachama.

Sera inatoa fursa kwa Wanachama kufahamu mambo ya kimiongozo yakiwemo:

a) Aina za Hisa na Akiba
b) Kima cha Chini cha Hisa
c) Utaratibu wa ukusanyaji na usimamizi wa Hisa na Akiba
d) Hisa na Akiba kama dhamana ya Mikopo
e) Urejeshaji wa Hisa na Akiba kwa Wanachama
f) Riba juu ya Akiba

Sera ya Hisa na Akiba imeandaliwa kwa ajili ya kukiwezesha Chama kutoa huduma kwa ufanisi kwa kuzingatia dhana ya uwazi, uwajibikaji, urahisi, na ulinzi wa mali za Chama na Wanachama.

### 2.2. Msingi wa Sera

Sera ya Hisa na Akiba imeandaliwa kwa kuzingatia: -

a) Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 na Kanuni zake
b) Masharti ya Chama
c) Sheria ya Kazi ya 2004
d) Sera na Kanuni za Fedha za Chama.
e) Mpango Mkakati wa Chama
f) Mahitaji ya Wanachama kupitia Mijadala na Maamuzi ya Mkutano Mkuu

## 2.3. Wigo wa Sera

Walengwa wakuu wa sera hii ni Wanachama.

## 2.4. Marekebisho ya Sera

a) Bodi ya Chama inaweza kufanya mapitio na maboresho ya Sera hii mara kwa mara ili kuendana na mabadiliko ya hali ya soko, mabadiliko ya Sheria husika, maoni na ushauri kutoka kwa wadau mbalimbali wa Ushirika, wakiwemo Wanachama ili kuleta ufanisi katika utendaji wa shughuli za ukusanyaji na usimamizi wa Hisa na Akiba katika Chama.

b) Mapendekezo yoyote ya marekebisho ya Sera hii yatawasilishwa katika Mkutano Mkuu wa Chama kwa maamuzi kabla ya kuanza kutumika rasmi.

## SEHEMU YA TATU

## HISA

### 3.1 Umiliki wa Hisa

a) Mwanachama mpya atakuwa na wajibu wa kununua Hisa za uanachama zisizopungua kiwango cha chini kilichowekwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali namba 1.

b) Kutakuwa na aina mbili za Hisa katika Chama: Hisa za lazima (Hisa za uanchama) na Hisa za hiari.

### 3.2 Kiwango cha Chini cha Hisa za Uanachama

a) Kila Mwanachama anayejiunga katika Chama kwa mara ya kwanza atahitajika kununua Hisa za uanachama kama ilivyoainishwa kwenye jedwali namba 1

b) Mwanachama ataweza kupata huduma katika Chama endapo atakuwa amenunua angalau nusu ya Hisa za uanachama.

c) Kiwango cha chini cha Hisa za uanachama kitakuwa kikibadilishwa kulingana na matakwa ya kisheria na mahitaji ya Chama

### 3.3 Utaratibu wa Ununuzi wa Hisa

a) Mwanachama atanunua Hisa kwa njia ya kukatwa kutoka kwenye mshahara wake au kulipa kupitia benki na kuwasilisha risiti ya malipo ya benki, kwenye ofisi ya Chama.

b) Mwanachama anaweza kununua hiza Hisa zaidi ya hisa za lazima za uanachama. Hiza hizi zitaitwa Hisa za hiari.

### 3.4 Uendeshaji wa Akaunti ya Hisa

a) Taarifa ya ununuzi wa Hisa zitaingizwa katika akaunti ya Hisa husika kwenye mfumo laini mara ofisi ipatapo uthibitisho wa malipo ya Hisa kufanyika.

b) Mara baada ya kukamilisha malipo ya hisa za uanachama, mwanachama anaweza kupewa atapewa cheti cha umiliki wa Hisa kitakachoandaliwa na chama, kwa utaratibu utakaowekwa.

### 3.5 Kuhamisha Hisa

a) Mwanachama hataruhusiwa kuhamisha Hisa zake za uanachama kwenda kwa Mwanchama mwingine isipokuwa Hisa za hiari.

b) Chama hakitaruhusiwa kuhamisha Hisa za mwanachama ama mtaji wa Chama kwenda kwenye taasisi nyingine.

### 3.6 Katazo la Kutumia Hisa kama Dhamana

Hisa za uanachama hazitatumika kwa namna yoyote ile kama dhamana ya mkopo kwa Mwanchama isipokuwa hisa za hiari

### 3.7 Kurejeshewa Hisa

3.7.1. Mwanachama atarejeshewa hisa zake za uanachama na za hiari, pale uanachama wake utakapokoma.

3.7.2. Marejesho ya Hisa yatafanyika ndani ya siku tisini (90) tangu kupokelewa kwa maombi ya kurejeshewa hisa.

3.7.3. Kabla ya marejesho ya Hisa za uanachama kufanyika, Mwanchama au msimamizi wa mirathi atatakiwa kurejesha cheti cha umilki wa Hisa wakati wa kuwasilisha maombi ya kurejeshewa.

### 3.8 Tathimini ya Thamani ya Hisa

Chama kitakuwa na utaratibu wa kufanya tathmini ya Hisa za uanachama kila baada ya miaka 3 ili kuhakikisha kuwa thamani ya Hisa za Wanachama zinaendana na hali halisi ya maendeleo ya Chama.

# SEHEMU YA NNE

# AKIBA

## 4.1 Aina ya Akiba Katika Chama

a) Chama kitakuwa na bidhaa za akiba zilizogawanywa katika makundi mawili (2) yaani akiba ya lazima na akiba ya hiari.

b) Kila Mwanachama atatakiwa kujiwekea akiba ya lazima kila mwezi kwa kuzingatia kiwango cha chini cha akiba kilichoaninishwa kwenye jedwali namba 1. Akiba hizi ni za lazima kwa kila Mwanachama kama ilivyoainishwa kwenye kifungu namba 13 cha Masharti ya Chama.

## 4.2 Akiba ya Lazima

### 4.2.1 Uhamasishaji

a) Katika kuhakikisha kuwa Chama kinakusanya fedha ya kutosha kwa ajili ya kutoa huduma bora na kwa wakati kwa Wanachama, uongozi wa Chama utajiwekea utaratibu wa kuhamasisha Wanachama kuongeza kiasi cha malimbikizo (deposits) ya akiba zao ndani ya Chama kwa manufaa yao ya sasa na ya baadae.

b) Uhamasishaji huu utalenga pia kushawishi wafanyakazi wa Mamlaka wasio Wanachama ili kujiunga na Chama.

c) Uhamasishaji utafanyika kwa njia ya utoaji huduma bora ya kuvutia, mikutano ya vituo, vipeperushi na TOVUTI ya Chama.

d) Kutakuwa na uhamasishaji endelevu katika kuhakikisha kuwa Chama kinakuwa na uwezo wa kifedha ili kuwa na ukwasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya Wanachama kwa wakati.

### 4.2.2 Utaratibu wa Uchangiaji

a) Kila Mwanachama atatakiwa kuchangia kila mwezi kiasi kisichopungua kiwango kilichowekwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali namba 1.

b) Mwanachama ataruhusiwa kuongeza au kupunguza kiwango cha uchangiaji wa akiba cha kila mwezi kulingana na uwezo wake wa kiuchumi pamoja na mahitaji yake.

c) Michango ya akiba ya kila mwezi kwa Wanachama walio ndani ya ajira ya Mamlaka itatakiwa kuwasilishwa kwenye Chama kupitia makato ya mishahara yao ya kila mwezi au kuweka bank standing order au kuweka pesa Benki (direct deposit) au kwa njia ya Simu.

d) Wanachama walio nje ya ajira ya Mamlaka watatakiwa kuandika *bank standing order* kuweka pesa Benki (direct deposit) au kwa njia ya Simu

ya makato ya michango ya akiba zao kila mwezi.

### 4.2.3 Riba Juu ya Akiba

a) Chama kitatoa riba juu ya akiba kila Mwaka kwa kuzingatia mapato ya Chama kwa Mwaka husika.

b) Kiwango cha chini cha riba (interest rate) juu ya akiba kitapangwa na Bodi ya Chama na kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kupitishwa.

c) Ukokotoaji wa riba ya akiba za Wanachama utakuwa ni kwa njia ya wastani uliopimwa (Weighted Average Method) kwa mwezi; kwa miezi kumi na mbili (12) ya mwaka husika.

d) Mwanachama atatakiwa kufanya maamuzi ya kulipwa riba ya akiba zake au kuiacha ili iongeze akiba zake kwenye Chama. Maamuzi haya yatafanywa kupitia *Members Portal*.

e) Mwanachama atapata taarifa juu ya riba aliyopata kwenye akiba zake kila mwaka kupitia *Members Portal*.

f) Kwa Wanachama watakaochagua kulipwa riba ya akiba zao, malipo yote yatafanyika kupitia akaunti zao za benki na taarifa ya malipo hayo itatolewa kwa Mwanachama kwa utaratibu ambao Chama kitaweka.

### 4.2.5 Uendeshaji wa Akaunti ya Akiba ya Lazima

a) Michango ya akiba ya lazima itaingizwa katika akaunti ya akiba ya Mwanchama husika kwenye mfumo laini mara ofisi ipatapo makato ya michango hiyo kutoka kwa Mwajiri au taarifa kutoka benki kwa wale walioweka michango yao moja kwa moja kwenye akaunti ya Chama.

b) Akiba ya lazima ndiyo itakuwa kigezo cha Mwanchama kupata huduma ya mkopo wa Maendeleo ya Jamii.

c) Akaunti ya akiba itahesabiwa kuwa mfu endapo Mwanchama hatachangia akiba ya kila mwezi kwa kipindi cha mwaka mmoja.

*d)* Mwanachama atapata taarifa juu ya mwenendo wa akaunti ya akiba zake kupitia *Members Portal.*

#### 4.2.6 Dhamana

Akiba ya lazima itatumika kama dhamana ya mkopo pale Mwanachama husika anapopewa mkopo katika Chama au pale ambapo Mwanachama amemdhamini Mwanchama mwingine.

#### 4.2.7 Kurejeshewa Akiba

(a) Akiba za lazima hazitarejeshwa kwa Mwanachama isipokuwa tu uanachama wake unapokoma.

(b) Bila kuathiri kifungu (a) hapo juu; Mwanachama anapofikia umri wa miaka 55 anaweza kurejeshewa kiasi kisichozidi asilimia 30 ya akiba yake ya lazima mara moja kwa mwaka; kwa kuzingatia kuwa salio la akiba yake baada ya kuchukua kiasi hicho halitakuwa pungufu ya mkopo alio nao.

(c) Marejesho ya Akiba ya lazima yaliyotajwa kwenye kifungu (b) hapo juu yatafanyika mara tu Chama kitakapopokea maombi ya kurejeshewa Akiba kwa njia ya maandishi kutoka kwa mwanachama.

(d) Endapo Mwanachama anakoma uanachama, marejesho ya Akiba yatafanywa ndani ya siku tisini (90) tangu kupokelewa kwa notisi ya maombi ya kurejeshewa akiba.

### 4.3 Akiba za Hiari

Mwanchama atajiunga au kujitoa kwenye Akiba za hiari pale atakapoamua yeye mwenyewe kulingana na masharti yatakayokuwa yamewekwa kwenye bidhaa husika za hiari bila kuathiri hali ya uanachama wake ndani ya Chama.

Kutakuwa na aina zifuatazo za akiba za hiari:

### 4.3.1 Akiba ya Kustaafu

#### 4.3.1.1 Utaratibu wa Kujiunga

a) Mwanachama atajiunga na uchangiaji wa akiba ya wastaafu kwa hiari yake mwenyewe kwa kujaza fomu maalum ya kujiunga na bidhaa hiyo inayopatikana kwenye tovuti au Ofisi ya Chama.

b) Katika kuhakikisha kuwa Wanachama wanafahamishwa umuhimu wa bidhaa hii, uongozi wa Chama utajiwekea utaratibu wa kuhamasisha Wanachama kujiunga na bidhaa hii kwa manufaa yao.

#### 4.3.1.2 Taratibu za Uchangiaji

a) Michango ya akiba ya kila mwezi kwa Wanachama walio ndani ya ajira ya Mamlaka itatakiwa kuwasilishwa kwenye Chama kupitia makato ya mishahara yao ya kila mwezi au kuandika bank standing order au kuweka pesa Benki (Direct deposit) au kwa njia ya Simu.

b) Mwanachama aliyejiunga na bidhaa hii atatakiwa kuchangia kiasi kisichopungua kile kilichoainishwa kwenye Jedwali namba 1.

c) Mwanachama ataruhusiwa kuongeza au kupunguza kiwango cha uchangiaji wa akiba cha kila mwezi kulingana na uwezo wake na mahitaji yake kwa kujaza fomu maalum kwa kusudio la kufanya hivyo.

*d)* Wanachama walio nje ya ajira ya Mamlaka watatakiwa kuandika *bank standing order au* kuweka pesa Benki (Direct deposit) au kwa njia ya Simu kuchangia michango ya akiba zao kila mwezi.

#### 4.3.1.3 Riba Juu ya Akiba

a) Chama kitatoa riba juu ya akiba hii kila mwaka kwa kiwango kilichoainishwa kwenye jedwali namba 1

b) Akiba katika bidhaa hii itastahili kupata riba baada ya kiasi cha akiba kwenye akaunti ya Mwanachama kufikia kiasi kilichoainishwa kwenye jedwali namba 1

c) Mabadiliko yeyote ya kiwango cha riba yatawasilishwa na Bodi kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kupitishwa.

d) Ukokotoaji wa riba ya akiba utakuwa ni kwa njia ya wastani uliopimwa (Weighted Average Method) kwa mwezi; kwa miezi kumi na mbili (12) ya mwaka husika.

e) Mwanachama atapewa taarifa juu ya riba aliyopata kwenye akiba zake kila mwaka kupitia *Members Portal.*

f) Mwanachama atatakiwa kufanya maamuzi ya kulipwa riba ya akiba zake au kuiacha ili iongeze akiba zake kwenye Chama. Maamuzi haya yatafanywa kupitia *Members Portal.*

g) Wanachama watakaochagua kulipwa riba ya akiba zao, malipo yote yatafanyika kupitia benki.

#### 4.3.1.4 Uendeshaji wa Akiba

a) Michango ya akiba ya wastaafu itaingizwa katika akaunti ya akiba ya Mwanchama husika kwenye mfumo laini mara ofisi ipatapo makato ya michango hiyo kutoka kwa Mwajiri au taarifa kutoka benki kwa wale walioweka michango yao moja kwa moja kwenye akaunti ya benki.

b) Mwanachama ataweza kupata taarifa ya michango ya akiba zake kupitia *Members Portal.*

c) Akiba hii haitatumika kama kigezo cha kutoa mkopo kwa Mwanchama bali inaweza kutumika kama dhamana ya mkopo.

#### 4.3.1.5 Dhamana

a) Akiba ya wastaafu itatumika kama dhamana ya mkopo pale Mwanachama husika anapopewa mkopo katika Chama.

b) Akiba ya wastaafu pia itatumika kama dhamana ya mkopo ambao Mwanachama amemdhamini Mwanachama mwingine.

#### 4.3.1.6 Kurejeshewa Akiba

a) Ikiwa Mwanachama anahitaji kupunguza sehemu ya akiba yake, Bodi inaweza kumruhusu kuchukua akiba isiyozidi asilimia 30 ya akiba zake zote mara moja kwa mwaka wakati akiendelea na uanachama na

sehemu ya akiba inayopunguzwa isiwe imetumika kama dhamana ya mkopo. Punguzo la akiba litalipwa mara tu Chama kitakapopokea maombi ya kupunguza akiba.

b) Akiba zitakazopunguzwa hazitalipwa riba juu ya akiba, riba italipwa kwenye salio la akiba mwisho wa mwaka.

c) Ikiwa Mwanachama anahitaji kurejeshewa akiba zake zote marejesho yatafanyika ndani ya siku tisini (90) tangu kupokelewa kwa notisi ya kuomba kurejeshewa akiba yake.

### 4.3.2 Akiba ya Elimu

#### 4.3.2.1 Utaratibu ya Kujiunga

a) Mwanachama atajiunga na uchangiaji wa akiba ya elimu kwa hiari yake mwenyewe kwa kujaza fomu maalum ya kujiunga na bidhaa inayopatika kwenye tovuti au ofisi ya Chama.

b) Katika kuhakikisha kuwa Wanachama wanafahamishwa umuhimu wa bidhaa hii, uongozi wa Chama utajiwekea utaratibu wa kuhamasisha Wanachama kujiunga na bidhaa hii kwa manufaa yao.

#### 4.3.2.2 Utaratibu wa Uchangiaji

a) Kila Mwanchama aliyejiunga na bidhaa hii atatakiwa kuchangia kiasi kisichopungua kiwango kilichoainishwa kwenye jedwali namba 1 kwa mwezi kama mchango wa akiba ya elimu.

b) Mwanachama ataruhusiwa kuongeza au kupunguza kiwango cha uchangiaji wa akiba cha kila mwezi kulingana na uwezo wake na mahitaji yake kwa kujaza fomu maalum ya kusudio la kufanya hivyo.

c) Michango ya akiba ya kila mwezi kwa Wanachama walio ndani ya ajira ya Mamlaka itatakiwa kuwasilishwa kwenye Chama kupitia makato ya mishahara yao ya kila mwezi au kuweka benki standing order au kuweka pesa Benki (Direct deposit) au kwa njia ya Simu.

d) Wanachama walio nje ya ajira ya Mamlaka watatakiwa kuandika *benki standing order* order au kuweka pesa Benki (Direct deposit) au kwa njia ya Simu kuchangia michango ya akiba zao kila mwezi.

#### 4.3.2.3 Riba Juu ya Akiba

a) Chama kitatoa riba juu ya akiba kwenye salio la akiba kila Mwaka kwa kuzingatia mapato ya Chama kwa Mwaka husika.

b) Kiwango cha chini cha riba (interest rate) juu ya akiba kitapangwa na Bodi ya Chama na kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya idhini ya kutumika.

c) Ukokotoaji wa riba ya akiba za Wanachama utakuwa ni kwa njia ya wastani uliopimwa (Weighted Average Method) kwa mwezi; kwa miezi kumi na mbili (12) ya mwaka husika.

*d)* Kila Mwanachama atapewa taarifa juu ya riba aliyopata kwenye akiba zake kila mwaka kupitia *Members Portal.*

~~e)~~ Mwanachama atatakiwa kufanya maamuzi ya kulipwa riba ya akiba zake au kuiacha ili iongeze akiba zake kwenye Chama. Maamuzi haya yatafanywa kupitia *Members Portal*

f) Kwa Wanachama watakaochagua kulipwa riba ya akiba zao, malipo yote yatafanyika kupitia benki

#### 4.3.2.5 Uendeshaji wa Akiba

a) Michango ya akiba ya elimu itaingizwa katika akaunti ya akiba ya Mwanchama husika kwenye mfumo laini mara ofisi ipatapo makato ya michango hiyo kutoka kwa Mwajiri au taarifa kutoka benki kwa wale walioweka michango yao moja kwa moja kwenye akaunti ya benki.

b) Mwachama ataweza kupata taarifa ya michango ya akiba zake kupitia *Members Portal*.

c) Akiba hii itatumika kama kigezo cha Mwanachama kupata mkopo wa elimu, ambapo Mwanachama ataweza kukopeshwa mkopo wa elimu usiozidi mara mbili (2) ya akiba ya elimu aliyonayo katika Chama.

d) Mwanachama ataruhusiwa kuongeza mkopo juu ya mkopo wa elimu alio nao (elimu top up) ilimradi jumla ya mkopo wake Pamoja na riba havitazidi mara mbili ya akiba zake katika mfuko wa elimu.

#### 4.3.2.6 Dhamana

a) Akiba ya elimu itatumika kama dhamana ya mkopo pale Mwanachama husika anapopewa mkopo katika Chama.

b) Akiba ya elimu pia itatumika kama dhamana ya mkopo ambao Mwanachama amemdhamini Mwanachama mwingine.

#### 4.3.2.6 Kurejeshewa Akiba

a) Mwanachama ataruhusiwa kurejeshewa kiasi cha akiba ya elimu aliyonayo katika Chama kwa kuzingatia kwamba salio la akiba zake halitakuwa chini ya kiwango kilichoainishwa kwenye jedwali namba 1.

b) Endapo Mwanachama ana mkopo wa elimu, ataruhusiwa kuchukua sehemu ya akiba yake kama salio la mkopo wake pamoja na riba havitazidi mara mbili ya akiba zake.

c) Mwanachama ataruhusiwa kuchukua sehemu ya akiba yake ya elimu mara moja kila robo mwaka. Marejesho haya yatafanyika mara tu Chama kitakapopokea maombi kutoka kwa mwanachama.

d) Ikiwa Mwanachama anahitaji kurejeshewa akiba zake zote marejesho yatafanyika ndani ya siku tisini (90) tangu kupokelewa kwa notisi ya kuomba kurejeshewa akiba yake.

### 4.3.3 Akiba ya Afya

#### 4.3.3.1 Utaratibu wa Kujiunga

a) Mwanachama atajiunga na uchangiaji wa akiba ya afya kwa hiari yake mwenyewe kwa kujaza fomu maalum ya kujiunga na bidhaa

b) Katika kuhakikisha kuwa Wanachama wanafahamishwa umuhimu wa bidhaa hii, uongozi wa Chama utajiwekea utaratibu wa kuhamasisha Wanachama kujiunga na bidhaa hii kwa manufaa yao.

#### 4.3.3.2 Utaratibu wa Uchangiaji

a) Kila Mwanachama aliyejiunga na bidhaa hii atatakiwa kuchangia kiasi kisichopungua kile kilichoainishwa kwenye Jedwali namba 1

b) Mwanachama ataruhusiwa kuongeza au kupunguza kiwango cha uchangiaji wa akiba cha kila mwezi kulingana na uwezo na mahitaji yake kwa kujaza fomu maalum kwa kusudio la kufanya hivyo

c) Michango ya akiba ya kila mwezi kwa Wanachama walio ndani ya ajira ya Mamlaka itatakiwa kuwasilishwa kwenye Chama kupitia makato ya mishahara yao ya kila mwezi au kuweka bank standing order au kuweka pesa Benk (Direct deposit) au kwa njia ya Simu.

d) Wanachama walio nje ya ajira ya Mamlaka watatakiwa kuandika *bank standing order* ya makato ya michango ya akiba zao kila mwezi

**4.3.3.3 Riba Juu ya Akiba**

a) Chama kitatoa riba juu ya akiba kila Mwaka kwa kuzingatia mapato ya Chama kwa Mwaka husika.

b) Kiwango cha chini cha riba (interest rate) juu ya akiba kitapangwa na Bodi ya Chama na kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya idhini ya kutumika.

c) Ukokotoaji wa riba ya akiba za Wanachama utakuwa ni kwa njia ya wastani uliopimwa (Weighted Average Method) kwa mwezi; kwa miezi kumi na mbili (12) ya mwaka husika.

d) Kila Mwanachama atapewa taarifa juu ya riba aliyopata kwenye akiba zake kila mwaka kupitia Members Portal.

e) Mwanachama atatakiwa kufanya maamuzi ya kulipwa riba ya akiba zake au kuiacha ili iongeze akiba zake kwenye Chama. Maamuzi haya yatafanywa kupitia member’s portal.

f) Kwa Wanachama watakaochagua kulipwa riba ya akiba zao, malipo yote yatafanyika kupitia benki na taarifa ya malipo hayo itatolewa kupitia kwa kiongozi wa kituo.

**4.3.3.4 Uendeshaji wa Akiba**

a) Michango ya akiba ya afya itaingizwa katika akaunti ya akiba ya Mwanchama husika kwenye mfumo laini mara ofisi ipatapo makato ya michango hiyo kutoka kwa Mwajiri au taarifa kutoka

benki kwa wale walioweka michango yao moja kwa moja kwenye akaunti ya Chama katika benki

b) Mwachama ataweza kupata taarifa ya michango ya akiba zake kwenye Chama kwa kuomba stetimenti ya akaunti ya akiba.

c) Akiba hii haitatumika kama kigezo cha Mwanachama kupata mkopo

**4.3.3.5 Dhamana**

Akiba ya afya itatumika kama dhamana ya mkopo pale Mwanachama husika anapopewa mkopo katika Chama au kumdhamini Mwanchama mwingine kuchukua mkopo.

**4.3.3.6 Kurejeshewa Akiba**

a) Mwanachama ataruhusiwa kurejeshewa asilimia mia moja (100%) ya kiasi cha akiba ya afya aliyonayo katika Chama

b) Marejesho ya akiba yatafanywa ndani ya siku tisini (90) tangu kupokelewa kwa notisi ya kuomba kuchukua sehemu ya akiba ya afya au kufunga akaunti ya akiba hiyo.

### 4.3.4 Akiba ya Wekeza

**4.3.4 .1 Utaratibu wa Kujiunga**

(a) Mwanachama atajiunga na uchangiaji wa akiba ya wekeza kwa hiari yake mwenyewe kwa kujaza fomu maalum ya kujiunga na bidhaa hiyo inayopatikana kwenye tovuti au ofisi ya Chama.

(b) Katika kuhakikisha kuwa Wanachama wanafahamishwa umuhimu wa bidhaa hii, uongozi wa Chama utajiwekea utaratibu wa kuhamasisha Wanachama kujiunga na bidhaa hii kwa manufaa ya kiuchumi na kijamii.

**4.3.4 .2 Taratibu za Uchangiaji**

(a) Kila Mwanachama aliyejiunga na bidhaa hii atatakiwa kuchangia kiasi kisichopungua kile kilichoainishwa kwenye Jedwali namba 1.

(b) Mwanachama ataruhusiwa kuongeza au kupunguza kiwango cha uchangiaji wa akiba cha kila mwezi kwa kujaza fomu maalumu.

(c) Michango ya akiba ya kila mwezi kwa Wanachama itatakiwa kuwasilishwa kwenye Chama kupitia makato ya mishahara yao ya kila mwezi au kuandika *benki standing order, au kwa njia ya simu au kwa kuweka pesa benki*.

(d) Ikiwa Mwanachama anataka kufanya mabadiliko juu ya kiwango cha uchangiaji kwa mwezi, atatakiwa kutoa taarifa kwa Mweneyekiti wa Chama juu ya kusudio la kufanya hivyo.

**4.3.4 .3 Riba Juu ya Akiba**

(a) Kiwango cha riba juu ya akiba ya WEKEZA kwa mwaka kitakuwa kama kilichoainishwa kwenye jedwali namba 1

(b) Riba italipwa baada ya kiasi cha akiba kwenye akaunti ya Mwanachama kufikia kiasi kilichoainishwa kwenye jedwali namba 1

(c) Ukokotoaji wa riba ya akiba utakuwa ni kwa njia ya wastani uliopimwa (Weighted Average Method) kwa mwezi; kwa miezi kumi na mbili (12) ya mwaka husika.

(d) Kila Mwanachama atapata taarifa juu ya riba aliyopata kwenye akiba zake kila mwaka kupitia Members Portal.

(e) Mwanachama atatakiwa kufanya maamuzi ya kulipwa riba ya akiba zake au kuiacha ili iongeze akiba zake kwenye Chama. Maamuzi haya yatafanywa kupitia Members Portal.

(f) Kwa Wanachama watakaochagua kulipwa riba ya akiba zao, malipo yote yatafanyika kupitia benki.

**4.3.4 .4 Uendeshaji wa Akiba**

d) Michango ya akiba ya WEKEZA itaingizwa katika akaunti ya akiba ya Mwanchama husika kwenye mfumo laini mara ofisi ipatapo makato ya michango hiyo kutoka kwa Mwajiri au taarifa kutoka benki kwa wale walioweka michango yao moja kwa moja kwenye akaunti ya benki.

e) Mwachama ataweza kupata taarifa ya michango ya akiba zake kupitia Members Portal.

f) Akiba hii haitatumika kama kigezo cha kutoa mkopo kwa Mwanchama, bali itaweza kutumika kama sehemu ya dhamana ya mkopo kwa Mwanachama au kwa kumdhanimi Mwanachama mwingine.

#### 4.3.4.5 Kurejeshewa Akiba

(a) Riba juu ya akiba ya WEKEZA iliyoainishwa kwenye jedwali namba 1 italipwa yote kwa mwanachama endapo akiba zake hazitapunguzwa kwa muda usiopungua miaka mitatu (3). Baada ya miaka mitatu kutimia, mwanachama atakuwa huru kuendelea au kutoendelea na wekezo la bidhaa hii.

(b) Endapo Mwanachama anahitaji kupunguza sehemu ya akiba yake ataruhusiwa kuchukua akiba lakini hatapa riba iliyoainishwa kwenye jedwali namba 1 bali atarejesha kwenye Chama nusu ya riba aliyokwishalipwa.

(c) Punguzo la akiba za WEKEZA litalipwa mara tu Chama kitakapopokea maombi ya kupunguza akiba.

(d) Endapo Mwanachama anahitaji kurejeshewa akiba zake zote katika bidhaa hii, marejesho yatafanyika ndani ya siku tisini (90) tangu kupokelewa kwa notisi ya kuomba kurejeshewa akiba yake.

## 5.0 Wanachama Wanaojitoa Katika Chama

Chama cha TRA SACCOS Ltd kama zilivyo taasisi nyingine za kifedha hufikia kipindi ambacho mwanachama anaweza kuhitaji kwa hiari yake kujitoa katika chama kutokana na sababu mbali mbali. Hivyo basi kwa kutambua hilo chama kimeweka utaratibu rasmi ambao mwanachama ataufuata ili kutimiliza azma yake.

Ili kujitoa Mwanachama atatakiwa kandika barua kwa mwenyekiti wa Chama ambayo ataeleza nia yake ya kujitoa na sababu kisha ataiwasilisha kwenye ofisi za Chama kwa ajili ya taratibu zinazofuata. Baada ya barua kupokelewa itafanyiwa kazi na kupitiwa na Bodi ya Chama na endapo itaridhiwa mwanachama atalipwa stahili zake ndani ya siku 90 tangu barua ya kujiondoa kupokelewa ikiwemo Hisa na Akiba zake, endapo atakuwa na mkopo atatakiwa kuulipa kabla maombi yake hayajakubaliwa.

## 5.1 Faida Anazopoteza Mwanachama Aliyejitoa

i. Mwanachama aliyejitoa uanachama anapoteza sifa za kuwa mwanachama na stahili nyingine kama mwanachama.

ii. Hupoteza riba ya Akiba endapo atakuwa amejitoa katikati ya mwaka kabla ya Mwaka kuisha, hii ni kwa kuwa riba hukokotolewa mara baada ya mwaka kuisha hivyo mwanachama akijitoa mapema kabla mwaka kuisha hupoteza riba hizo katika akiba. Kwa kuwa akaunti hufungwa mara tu baada ya kulipwa hisa zake na akiba.

iii. Hupoteza fursa ya kushiriki vikao vya chama na maamuzi mbalimbali juu ya chama.

iv. Mwanachama aliyejiondoa uanachama akaunti zake zote hufungwa na kusimamishwa miamala yoyote katika akaunti hizo.

## 6.0 Wanachama Waliosinzia

Chama cha TRA SACCOS LTD kinatambua kuwa katika kuendesha shughuli zake za ushirika kuna wanachama walio hai ambao huchangia akiba zao katika chama kila mwezi na hukopa kwa maendeleo na Ustawi wa Chama. Aidha kwa kutambua hilo pia kuna wanachama baadhi ambao huwa waliosinzia (Dormant) wanachama hawa waliosinzia ni wale ambao hawajafanya muamala wowote wa aidha kuchangia akiba, kukopa au kushiriki mikutano ya chama kwa muda wa miezi kumi na mbili kwa Mujibu wa Kanuni namba 62(1) ya vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo ya mwaka 2014.

Chama kitaanzisha Akaunti maalum kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zote za akaunti zilizosinzia. Baada ya kutenga kama akaunti zilizosinzia hatua zifuatazo zitazingatiwa

i. Baada ya akaunti kuwa iliyosinzia (Dormant) itapoteza sifa ya kuzalisha riba katika akiba hizo za mwanachama aliyesinzia.

ii. Chama kitachukulia akaunti zimetelekezwa endapo mwanachama husika au mwakilishi wake kisheria atakuwa hajawasiliana na SACCOS yeye binafsi au kwa maandishi ndani ya kipindi cha miaka mitano, ama kutoonesha nia kwenye fedha husika.

iii. Endapo fedha zitachukuliwa kuwa zimetelekezwa, kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2), SACCOS itapaswa kutoa notisi ya siku tisini kwa mwanachama au mwakilishi kupitia anwani ya mwanachama husika iliwayosilishwa kwa mara ya mwisho kuwa akaunti husika itafungwa na fedha zake kuhamishiwa kwenye akaunti ya mfuko wa matengo ya SACCOS.

iv. Endapo mwakilishi wa kisheria amepatikana lakini siyo mwanachama mwenyewe, Bodi inaweza kuhamisha fedha husika zilizotelekezwa kwa mwakilishi huyo.

v. Endapo mwanachama au mwakilishi wake wa kisheria hataweza kupatikana, Bodi kwa idhini ya Mkutano Mkuu wa mwaka inaweza kuhamishia fedha hizo kwenye akaunti ya mfuko wa matengo ya SACCOS na mwanachama au mtu yeyote mwenye maslahi atajulishwa kwa notisi kuhusu hatua iliyochukuliwa kupitia anwani ya mwisho inayofahamika.

vi. Endapo mwanachama sinzia atarejea na kuwasiliana na SACCOS kuhusu akaunti yake sinzia, SACCOS itaifufua akaunti yake na kurejesha bakaa yake kama ilivyokuwa awali.

**Jedwali namba 1**

| NA. | MAELEZO | KIASI (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Kiwango cha chini cha Hisa za uanachama kitakuwa Hisa 30 zenye thamani ya Shilingi 20,000 kila moja | 600,000 |
| 2 | Kiwango cha chini cha uchangiaji wa Akiba ya lazima kwa mwezi kwa kila Mwanachama | 50,000 |
| 3 | Kiwango cha chini cha uchangiaji wa Akiba ya hiari kwa mwezi kwa kila Mwanachama (Wastaafu, Elimu, Afya, WEKEZA) | 50,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Kiwango cha chini cha Akiba ya Elimu | 200,000 |
| 5 | Kiwango cha Chini cha akiba ya Wastaafu na WEKEZA | 500,000 |
| 6 | Riba juu ya Akiba ya Wastaafu na WEKEZA | 7% kwa mwaka |
| 7 | Riba juu ya Akiba ya Afya na Elimu | 3% kwa mwaka |
| 8 | Riba juu ya Akiba ya lazima | 3% kwa mwaka |
| | | |

**TRA SACCOS LTD** **OFISI YA MRAJISI**

________________________________

Pilly Marwa

Mwenyekiti TRA SACCOS LTD